# Kila mmoja wetu anaweza kufanya nini?

Chaguo rahisi katika maisha yetu ya kila siku zinaweza kuleta mabadiliko.

### Usinyamaze

Unga mkono hatua za kukabili mabadiliko ya tabianchi na matumizi ya nishati safi katika kiwango cha mtaa, jimbo na kitaifa.

Shiriki tunapoweka mipango ya kuboresha tabianchi ya jumuiya yetu na uwe sehemu ya wale watakaosaidia kuleta suluhu!

### Panda mimea na ulinde ile iliyoko

Miti husaidia kupunguza mabadiliko ya tabianchi na huwa na manufaa zaidi kwa jumuiya zetu, kama vile kusafisha hewa na maji.

### Nunua bidhaa kwa busara na uzirejelee tena na tena

Nunua bidhaa zinazodumu kwa muda mrefu, zinazorejelewa na zinazotumia nishati kidogo. Pia, fahamu kinachoweza na kile kisichoweza kurejelewa.

### Punguza matumizi ya nishati

Tumia balbu za LED na uzime taa na vifaa wakati havitumiki!

### Tumia nishati safi

Tumia balbu za LED na uzime taa na vifaa vya nyumba wakati havitumiki!

### Badilisha mbinu yako ya usafiri

Usafiri wa umma, wa pamoja, wa baiskeli, au kutembea husaidia kupunguza gesi kutoka kwa mbinu za usafiri, ambacho ni kiwango kikubwa na kinachoongezeka cha gesi zinazotolewa ulimwenguni.

## Je, ungependa kupata maelezo zaidi? Tembelea:

- Mikakati ya Kukabili Mabadiliko ya Tabianchi ya Erie County - **www.erie.gov/climateaction**
- Idara ya Mazingira na Mipango ya Erie County - **www.erie.gov/sustainability**
- Mikakati ya Kukabili Mabadiliko ya Tabianchi na Mpango Endelevu wa Uendeshaji wa Ndani wa Erie County - **www.erie.gov/CASP**
- Erie County Yaunga Mkono Ripoti ya Paris - **www.erie.gov/Paris**
- Mpango wa Nishati Endelevu kwa Watu wenye Mapato ya Chini wa Erie County - **www.erie.gov/ECLIPSE**
- Live Well Erie -**www.erie.gov/livewellerie**
- Tathmini ya Athari za Tabianchi - **www.erie.gov/cva**
- Sheria ya Kudibiti Tabianchi na Ulinzi wa Jamii katika Jimbo la New York - **www.climate.ny.gov**
- Shirika la Afya ya Umma ya Marekani "Jinsi Mabadiliko ya Tabianchi Yanavyoathiri Afya Yako" -**https://www.apha.org/ news-and-media/multimedia/infographics/how-climate-change-affects-your-health**
- "Mabadiliko ya Tabianchi 101 katika Climate Health Connect: Ripoti ya Misingi ya Sayansi ya Tabianchi" - **https://climatehealthconnect.org/wp-content/uploads/2016/09/Climate 101.pdf**
- Jopo la Kimataifa la Ripoti ya Mabadiliko ya Tabianchi ya 2018 - **www.ipcc.ch/sr15/**
- Majibu yote yasiyo ya Kiingereza yanaweza kutumwa kwa **sustainability@erie.gov** na tutahakikisha kuwa yatatafsiriwa na kujumuishwa katika mijadala yetu. Tunaomba radhi kwa usumbufu.

Ilisasishwa 03.2022


# MABADILIKO YA TABIANCHI

## Ni tatizo lililopo. Linatokea hapa tulipo.

Je, Erie County inachukua hatua gani? **www.erie.gov/climateaction**

### Tatizo ni gani?

Kuna ongezeko la gesi joto kwenye sayari yetu. Hali hii inabadilisha sana tabianchi hapa Magharibi mwa New York, na watu binafsi na jumuiya wanaathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kwa njia mbalimbali.




### Je, mabadiliko ya tabianchi yanaathiri aje eneo letu?

Ingawa athari hazionekani kila wakati, athari za mabadiliko ya tabianchi zinaweza kuonekana hapa Magharibi mwa New York. Mabadiliko ya tabianchi tayari yanasababisha dhoruba kubwa zaidi katika eneo letu, mawimbi hatari ya joto, kuongezeka kwa mafuriko, upepo mkali, kuongezeka kwa idadi ya wadudu na magonjwa. Mabadiliko haya yanaathiri kazi zetu, afya na mazingira yetu mazuri.



### Mafuriko


Kuongezeka kwa mvua, kuyeyuka kwa theluji na wastani wa kiwango cha mvua kwa miaka thelathini. Dhoruba kali zitaongezeka.



### Kuongezeka kwa Joto

Halijoto itaongezeka kwa wastani wa digrii 3-5 Fahrenheit kufikia katikati ya karne hii.

Viwango vya joto vilivyo juu humaanisha kupungua kwa kiwango cha barafu, hivyo kusababisha kunyesha theluji. Pia, mawimbi ya joto ya mara kwa mara yanatarajiwa.



### Spishi Vamizi na Magonjwa Yanayoambukizwa na Wadudu

Mbu, kupe, maradhi ya lyme, na mwani zitaongezeka zaidi tabianchi inapoendelea kubadilika.



***Hebu tushirikiane tulete mabadiliko!***

# Je, kuna hatari gani kwa eneo letu katika siku zijazo?

### Mazingira

Mwani hatari zaidi hujaa katika Ziwa Erie.



Hatari kubwa ya spishi vamizi huko Ziwa Erie.



Dhoruba kali zaidi na mafuriko ya mara kwa mara.



### Uchumi

Kuongezeka kwa mvua na mafuriko huleta hatari kubwa kwa nyumba na miundombinu.




Mazingira yanayobadilika yanaweza kuwa na athari mbaya kwa kazi na biashara zetu.




### Health

Kuongezeka kwa Magonjwa yanayoenezwa na wadudu na yanayotokana na kula chakula chenye viini vya magonjwa.

Athari za kiafya kutokana na hali mbaya ya hewa.




Kuongezeka kwa hatari kwa watu walio na pumu na ugonjwa wa moyo kutokana na hewa chafu na siku nyingi za ozoni.

Erie County CLIMATE ACTION

Kaunti ya Erie imejitolea kuunda jamii yenye Mpango wa Mikakati ya Kukabili Mabadiliko ya Tabia Nchi **unaozingatia usawa** Mpango unaoshughulikia athari hasi zisizo sawa kwa jamii zilizotengwa kihistoria. Kubuni na kutekeleza mipango ambayo husaidia wakazi wetu walio kwenye hatari zaidi kutaleta manufaa kwa jumuiya nzima.

## Kwa nini tunapaswa kuchukua hatua sasa kuhusu mabadiliko ya tabia nchi?

Kuongezeka kwa chaguo za usafiri wa kikanda hupunguza uchafuzi wa mazingira na kuboresha ubora wa maisha.

Kwa kutumia nishati safi kwenye shughuli za kiuchumi inakuza ubunifu na ajira zinazotunza mazingira.



Kujenga kwa kutunza mazingira hufanya nyumba zetu, biashara, na maeneo yetu ya kazi kuwa yenye afya zaidi na hupunguza gharama za matumizi.

Kujitayarisha kwa mabadiliko ya tabia nchi hutufanya tuyastahimili zaidi matukio kali ya hali ya hewa.

Kuhifadhi rasilimali na kupunguza matumizi mbaya ya rasilimali huokoa pesa sasa na katika siku zijazo.

Kukabili mabadiliko ya tabianchi italeta manufaa kwa afya yetu, mazingira, na uchumi.

***Husika!*** • **www.erie.gov/climateaction/participate**

# Je, Erie County inachukua hatua gani sasa?

Erie County imejitolea kushughulikia mabadiliko ya tabianchi.
Baadhi ya miradi ambayo tumetekeleza ili kupunguza utoaji wa gesi chafu ni pamoja na:

### Usafiri

Kupitia mpango wa NYSERDA NY wa Kuweka Vituo vya Nishati, Kaunti imeongeza maeneo 10 mapya ya kuweka nishati kwa magari katika Kaunti nzima. Maeneo haya mapya ni pamoja na bustani nyingi na viwanja vya gofu vinavyomilikiwa na Kaunti, na vyuo vikuu vya ECC. Kaunti pia inaangazia kutengeneza miundombinu ya kuweka nishati kwa haraka.

NFTA-METRO

Erie County imekuwa ikiunga mkono kuongezwa kwa msaada wa kifedha kutoka kwa jimbo kwa Eneo la Niagara Mradi wa Mamlaka ya Usafiri (NFTA) wa Upanuzi wa Reli ya Metro.

Erie County ilihusika kikamilifu katika kuandaa Mpango wa Uendeshaji Baiskeli katika Eneo Kubwa la Niagara, Mpango unajumuisha malengo na shabaha ya kusaidia kuunda jumuiya nyingi zinazoweza kuendesha baiskeli katika eneo letu.

### Nishati

Mpango wa Nishati Endelevu kwa Watu Wenye Mapato ya Chini katika Erie County (ECLIPSE) - Familia zenye mapato ya chini na wastani hutumia asilimia kubwa ya mapato yao kulipa gharama za nishati na mara nyingi haziwezi kutumia mbinu za kupunguza gharama za nishati kwa kutumia nishati inayoweza kutumika tena. ECLIPSE itashughulikia athari hizi kwa familia ambazo zinastahiki Mpango wa Usaidizi wa Nishati ya Nyumbani (HEAP) ikilenga ununuzi wa nishati nyingi na safi, utoaji wa nishati ya jua kwa jamii na moboresho ya ubora na uthabiti wa nishati husika.

Erie County ilishirikiana na Shirika la WNY Sustainable Business Roundtable kutoa nishati ya jua kwa biashara zilizo wanachama wake, ikiwa ni pamoja na Wafanyakazi wa Erie County. Kampeni hiyo ilikamilika mnamo Februari 2018, ikiwa imewezesha uwekaji wa kilowati 185 za nishati ya jua kwa nyumba za wafanyakazi, na kusababisha uepukaji wa kuzalishwa kwa tani 66 za GHG kila mwaka.

### Mazingira

Erie County imeendelea kuwa katika mstari wa mbele katika uhifadhi na uboreshaji wa mazingira kando ya Mto Buffalo. Eneo hili ambalo awali Lilikuwa na Viwanda vingi limeboreshwa kwa njia kubwa katika usafi wa maji na urejesho wa usafi wa maji haya kwa wanyama wa majini. Kazi hii ilijumuisha urekebishaji, urejeshaji, na ufufuaji wa maeneo matatu ya bustani, ikijumuisha Thomas F. Higgins Bridge na Riverfront, Park (Bailey Peninsula Natural Habitat Park), Red Jacket Natural Habitat Park and Seneca Bluffs Natural Habitat Park.

Bustani za Erie County zilianza kutekeleza mikakati ya kukata nyasi kwa kiwango kidogo au kutokatwa kabisa kwa nyasi, kwa mujibu wa Usasishaji wa Mpango wa Uhifadhi wa Bustani za kaunti, na pia inazingatia ushirikiano na mradi wa Uhifadhi wa Mazingira wa Woodland, ambao unaweza kutoa rasilimali kubuni mpango wa usimamizi.

ERIE COUNTY PARKS DEPT. NY

## Mpango wa Mikakati ya Kukabili Mabadiliko ya Tabianchi:

Erie County ilibuni Mpango wa Uendelevu na Mikakati ya Kukabili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Shughuli za ndani ulioidhinishwa na Bunge mnamo Februari, 2019. **www.erie.gov/CASP**

***Mpango huu una maeneo sita lengwa:*** Usafiri, Majengo na Nishati, Udhibiti wa Utupaji Taka na Urejeshaji, Usimamizi wa Ardhi, Maji, na Ununuzi.